SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.20 NO. 1 2021
DOI: 10.51984/JOHS.V20I1.1524

جامعة سبها للعلوم الإنسانية مجلة
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: https://sebhau.edu.ly/journal/index.php/johs

# Uyakinishi Na Ukanushi Katika Kiswahili

Mohammed. E. M. A. Taher

Department of Languages and African Studies, Faculty of Arts, Sebha University, Libya

**Keywords:**
Uyakinishi
Kukubali
Kiambiahi
Njeo
Kitenzi

**ABSTRACT**

Lugha ni aina ya sauti ambazo watu wa lugha fulani hutumia kuwasiliana katika jamii. Lugha yoyote ya ulimwengu imejengwa na aina ya viambishi awali, kama Profesa (Kihore) ambaye amebobea katika sayansi yangu alisema: mofolojia na sarufi katika lugha ya Kiswahili: Mofimu inayohusiana na mzizi ni neno linalowakilisha kesi, au maana tofauti , na viambishi awali vina umuhimu maalum katika lugha ya Kiswahili.Kuna viambishi vinavyoelezea Hali ya kukanusha, uthibitisho wa nyakati tofauti, na athari ya kitenzi kikuu baada ya kuingia kwa mofimu ya kukanusha katika muundo halisi wa Lugha ya Kiswahili.

# النفى والإثبات فى السواحلية

محمد إمحمد محمد على الطاهر

قسم اللغات والدراسات الإفريقية، كلية الآداب، جامعة سبها، ليبيا

**الكلمات المفتاحية:**
نفى
إثبات
بادئة
زمن
فعل

**الملخص**

اصبحت اللغة هي شكل من الأصوات الذي يستخدمه أهل لغة معينة للتواصل في مجتمع ما. إن أي لغة من لغات العالم تبنى بأنواع من البادئات كما قال البروفيسور (Kihore) المتخصص في علمي: الصرف، والنحو في اللغة السواحلية: إن المورفيم المرتبط بالجذر كلمة تنوب عن حال، أو معنى مختلف، والبادئات تحمل أهمية خاصة في اللغة السواحلية توجد بادئات توضح حالة النفي،والإثبات للأزمنة المختلفة،وتأثير الفعل الأساسي بعد دخول مورفيم النفي في التركيب الفعلي في اللغة السواحلية.

## Utangulizi

Lugha ni mfumo wa sauti za nasibu uliokubaliwa na watumizi wa lugha fulani katika mawasiliano yao ya kijamii.
Lugha yoyote duniani hujengwa kwa viambishi anuwai, katika kuvitolea ufafanuzi Kihore na wenzake (2003) amesema ni mofimu zinazogunganishwa katika mzizi wa neno ili kuwakilisha hali au dhana mbali mbali zinazoambatanishwa na neno pamoja na mofimu hizo, hata hivyo mfuatano wa viambishi hutafautiana kutoka lugha moja na nyingine. Viambishi huundwa kwa sauti moja au zaidi zenye kubeba dhima maalum. Katika lugha ya Kiswahili kuna viambishi vyenye kuonyesha hali ya kukubali na ukanushi.'Katika lugha ya Kiswahili dhana ya ukanushi na kukubali inajitokeza katika nafsi na njeo. Kukubali ni hali ya kuridhia jambo na ukanushi ni hali ya kukataa jambo.

. **VIAMBISHI NAFSI VYA UYAKINISHI**

Kulingana na zungumza Kiswahili hatua ya kwanza amevitaja viambishi vya uyakinishi kuwa ni:-

Ni
U
A
TU
M
WA

Kulingana na kitabu hicho **Ni** – inawakilisha nafsi kwanza umoja.
Kwa mfano:
**Ni**nasoma
Ni- inawakilisha nafsi ya kwanza umoja.
U- inawakilisha ya pili umoja.
A- inawakilisha nafsi ya tatu umoja.
Tu- inawakilisha nafsi ya kwanza wingi.
M- inawakilisha nafsi ya pili ya umoja.

*Corresponding author:
E-mail addresses: Moh.tah@Sebhau.edu.ly
*Article History : Received 30 March 2021 - Received in revised form 15 April 2021 - Accepted 30 June 2021*

Wa- inawakilisha nafsi ya tatu wingi.

**UYAKINISHI KWA VITENZI SHIRIKISHI.**

Kulingana na Mohammed (2001) ameonyesha Vitenzi shirikishi kadhaa ambavyo ni: **Ni-, –li-, ndi , -na, –po, -ko, -mo**, **U** na **yu** n.k. Kulingana na maelezo yake vitenzi hivi hufanya kazi kama vitenzi vikuu vikiashiria uyakinishi. Kulingana na ufafanuzi wake kishirikishi **Ni** kinaelezea sifa ya mtu au kitu. Ashton (1982) anakielezea kishirikishi hiki kama ni kionyeshi cha kubashiria dhana bila ya kitenzi, anaendelea kusema kwamba kishirikishi hiki kinatumika kuonyesha wakati wa sasa kwa mfano:

i) Kunguru **ni** ndege hodari
ii) Libya **ni** nchi kubwa

Pia anafafanua kuwa kishirikishi **Ni** kinaweza kusimama mwanzo wa sentensi. Katika mazingira kama haya **Ni** inaonyesha hali ya msisitizo wa jambo mfano:

i) **Ni** yeye anayepika sana
ii) **Ni** vitu vyetu vilivyopotea

**Ndi** – ni kionyeshi cha – **O**- ya urejeshi Mohammed anaelezea kuwa kirejeshi hiki kinatumika kuonyesha msisitizo wa kishirikishi aidha kishirikishi **Ndi** – kinabeba dhana ya uyakinishi na kinabadilika kulingana na Ngeli za majina. Hii ina maana kuwa kishiriki hiki hubeba urejeshi na kujitokeza katika maumbo tofauti kulingana na Ngeli za majina. Katika kuthibitisha dhana hii Mohammed anatuonyesha mifano ifuatayo:-

i) Huyu **ndiye** mwizi mwenyewe
ii) Kitabu kile **ndicho** kibovu
iii) Wale **ndio** wahalifu wenyewe
iv) Vikombe hivi **ndivyo** vipya
v) Hapa **ndipo** anapolala

-**Li-** Mohammed ameonyesha kuwa kishirikishi **Ni**, ni kionyeshi katika sentensi zenye muundo wa uhusishi, katika hali ya kukubali. Kishirikishi hili kwa ujumla wake kinarejelea wakati wa sasa. Kishirikishi hiki kwa kiasi fulani ni tafauti na njeo ya wakati uliopita **li**. Kimuundo kishirikishi –**li**- hufuatwa na kiambishi rejeshi, mifano ifuatayo inadhihirisha muundo wa kishirikishi –**li**-

(i) A**liye**bahili hataishi kwa raha duniani
(ii) Wa**lio** wanafunzi hapa ni wawili tu
(iii) Kitabu ki**licho**changu ni hiki

Mohammed anaendelea kusema kishirikishi **–li-** kinaweza kufanya kazi pamoja na kishirikishi -**Si** -cha kukataa, katika kuelezea hali ya ujumla bila ya kuelezea mtu au kitu mahsusi.

i) Aliye si tajiri hapati kuishi kwa raha
ii) Walio si walimu wazuri hawawezi kuwafundisha wanafunzi hawa. Pia Mohammed ameeleza kuwa kishirikishi **–li-** kinafanya kazi pamoja na baadhi ya vielezi ili kuonyesha makali na hali fulani kwa mfano:-
   i. Nilipo ni pachafu
   ii. Tulivyo ni watu wakweli tu

**-Po,** kishirikikishi kinajitokeza katika muundo wa uhusishi kwa mfano

i) Aliyepo hapa ni mwanafunzi
ii) Waliokuwapo pale jana ni vijana wawili.

-**Ko**

Kulingana na Mohammed –**ko-** kiungama cha mahali kisichoonyesha mahali maalumu, kwa kawaida kiungami hiki hufuatwa nyuma na kiambishi nafsi. Mfano

i) Tuko huku
ii) Tuliokuwako kule jana ni wengi sana

Pia kinaweza kujitokeza katika muundo wa sentensi husishi, ambapo kishirikishi **Ko**- hufanya kazi sawa sawa katika sentensi zilizotangulia.

Aidha **-mo** ni kiunganishi cha mahali kinachoonyesha mahali, kishirikishi kinajitofautisha na – **ko**, kwa sababu –**mo** inaonyesha kitu kilichomo ndani, mfano:

i) Mgeni yumo bafuni
ii) Wale vijana wamo chumbani.

Ashton (1982) **–po, - ko**, na **–mo** ni viambishi vya mahali ambavyo vinafanya kazi kama viunganishi vya vielezi

**-Na**

Mohammed, ameeleza kielezi kushirikishi kikiungana –**Na** ya uhusishi pia kinafanya kazi kama kitenzi kishirikishi, kikionyesha kwa mfano:

i) Pana ghasia nyingi hapa

Katika sentensi hii, neno pana linaonyesha ukaribu wa mahali husika.

ii) Kuna mvua kubwa nje

Katika sentensi hii neno nje, limeashiria mahali mbali na alipo mzungumzaji

iii) Mna wageni wachache ukumbini

Katika sentesi hii neno mna linamaanisha wageni wamo katika mazingira ya ndani.

**--Yu**, kishirikishi –yu, kinafanya kazi kama kirai ambacho kinaelezea sifa maalum kwa mtu wa tatu umoja.

Mfano

i) Kijana Yule **yu** mshari sana
ii) Mwalimu wetu **yu** mpole

Katika sentensi hizi mbili kishirikishi –yu, kinasimama kama ni kitenzi na mara nyingi kinafuatwa na vivumishi kwa mfano katika sentensi hizi neno mpole na mshari yanaelezea sifa ya mtajwa.

**-U**

Kishirikishi **U**, kinafanya kazi wakati kitangulizi ni mtenda katika hali ya umoja. Kulingana na Mohammed vitangulizi hivi vinaweza kufanya kazi kwa vitu visivyo na uhai vikirejelea umoja katika Ngeli ya **M- Mi-** na **U-N** Mfano:

i) Wewe **u** mkaidi sana
ii) Mlango **u** mdogo
iii) Ukuta **u** mrefu

Katika sentensi hizi **U** inasimama kama kitenzi kikuu katika hali ya uyakinishi.

Mtafti amebaini kuwa kishirikishi **U** mara nyingi hufuatwa na vivumishi. Kama inavyoonekana katika mifano ya juu.

Mohammed ameendelea kusema pia kishirikishi **U** nafasi yake inaweza kuchukuliwa na **Ni.**

Tuangalie mifano ifuatayo:

i) Wewe **ni** mkaidi sana
ii) Mlango **ni** mdogo
iii) Ukuta ule **ni** mrefu

Kitenzi **kuwa** katika uyakinishi

Katika lugha ya Kiswahili **kuwa** ni kitenzi muhimu sana kinachotumiwa katika nyakati tofauti. Kitenzi hiki kinaweza kujitokeza katika maumbo tafauti kulingana na wakati na Muktadha.

**Kuwa katika wakati wa sasa**

Katika wakati wa sasa kuwa hujitokeza katika umbo la **Ni**. Kulingana na Zungumza Kiswahili Hatua ya Kwanza

**Ni-** inatumika katika

i) Kujitambulisha kwa kutaja jina la mtu.
ii) Kuonesha utaifa
iii) Kazi.

Kwa mfano:-

i) Mimi ni Ahmed
ii) Mohammed ni Mlibya
iii) Mimi ni mwalimu

Katika muktadha huu kitenzi **Ni** kinafanyakazi kama kitenzi kikuu ikitanguliwa na viwakilishi nafsi au Nomino. Nomino hizi zinaweza kuwa ni Nomino za pekee kwa mfano majina ya Watu, majina ya Nchi kwa mfano: Katika hali ya Umoja na Wingi

i) Libya ni nchi ya Kiafrika
ii) Libya na Misri ni nchi za Kiafrika
iii) Walibya ni Mashujaa

Mbali na kuonyesha majina, Utaifa na kazi, kinaweza kuonyesha tarehe, siku na hali

i) Leo **ni** Alhamis
ii) Leo **ni** tarehe 3
iii) Mini **ni** mgonjwa.

Kitenzi **kuwa** katika wakati uliopita kati wakati uliopita kitenzi kuwa hutanguliwa na **li** na kufanya umbo la l**i+** kuwa -------**likuwa**

Wakati wa ujao

Katika wakati ujao kitenzi kuwa hutanguliwa na **ta** na kufanya ula la ta+ kuwa
-----**takuwa.**

Aidha wakati enedelevu kitenzi hiki hupemba **me** na kufanya umbo la **me +** kuwa
----- **mekuwa.**

Kiambishi li katika wakati uliopita kiambishi **ta** katika wakati ujao na kiambishi **me** katika wakati endelevu vimetumika katika kuashiria wakati kitendo kilipotokea. Kwa mnasaba huu maumbo haya hutanguliwa na viambishi vya ngeli kwa mfano.

**Jadweli (a)**

| **Ngeli** | **-likuwa** | **-takuwa** | **-mekuwa** |
|---|---|---|---|
| A (Umoja ) | Alikuwa | Atakuwa | Amekuwa |
| Wa (Wingi) | Walikuwa | Watakuwa | Wamekuwa |
| KI | Kilikuwa | Kitakuwa | Kimekuwa |
| VI | Vilikuwa | Vitakuwa | Vimekuwa |
| U (M) | Ulikuwa | Utakuwa | Umekuwa |
| I (MI) | Ilikuwa | Itakuwa | Imekuwa |
| U (U) | Ulikuwa | Utakuwa | Umekuwa |
| Z (N) | Zilikuwa | Zitakuwa | Zimekuwa |
| I (N) | Ilikuwa | Itakuwa | Imekuwa |
| ZI (N) | Zilikuwa | Zitakuwa | Zimekuwa |
| LI ( JI) | Lilikuwa | Litakuwa | Limekuwa |
| YA (MA) | Yalikuwa | Yatakuwa | Yamekuwa |
| PA | Palikuwa | Patakuwa | Pamekuwa |
| KU | Kulikuwa | Kutakuwa | Kumekuwa |
| MU | Mulikuwa | Mutakuwa | Mumekuwa |

**Njeo za lugha ya Kiswahili**

Katika lugha ya Kiswahili, kuna njeo tano muhimu, Njeo hizi ni:- **Na, Me, Li, Ta** na **Hu**. Kulingana na Wilson Njeo ya **'Na'** inatumika kubainisha wakati wa sasa, wakati wa kuendelea na wakati wa mazoea.

Wakati wa sasa
Mfano:

i) Mtoto anakula wali

Katika sentensi hii kiambishi cha njeo -**na-** kinaashiria wakati wa sasa na pia wakati unaoendelea.

**'Me'** ni njeo inayobainisha wakati endelevu
Mfano:
Mwanafunzi amesoma kitabu.
Pia **'me'** inatumika kuonyesha hali katika wakati wa sasa
Mifano:

i) Tumechoka badala ya kusema Tunachoka
ii) Amelala badala ya kusema Analala

Wakati wa **'li'**
Njeo ya kiambishi **'li'** inaonyeha wakati uliopita.
Kwa mfano

i) Amina alikula mkate
ii) Yeye alifanya kazi

Njeo ya wakati ujao (**ta**)
**'Ta'** ni njeo inayoonyesha matarajio ya mtu au wakati ujao.
Mfano:

i) Nitaenda Libya
ii) Wageni wengi watajifunza Kiswahili Zanzibar

Njeo ya **Hu-**
Njeo ya **hu-** huonyesha kitendo kinachofanyika kila siku

Mifano:

i) Mimi hula chapati kila asubuhi
ii) Yeye huenda sokoni kila siku

Njeo ya **hu-** hutanguliwa na viwakilishi nafsi au majina
Mfano:
Mimi, wewe, yeye, sisi, nyinyi na wao.
Kama mifano ya juu inavyoonekana kimuundo njeo **Na, Me, Ta,** hupachikwa baada ya viambishi nafsi au ngeli za majina na kufuatiwa na mzizi wa neno.
Mfano:
Tuangalie jadweli ifuatayo:

**Jadweli (b)**

| | | |
|---|---|---|
| NI | NA | anguka |
| U | ME | soma |
| A | LI | imba |
| TU | TA | fanyakazi |
| WA | | zungumza |

Hata hivyo muundo huu, haujitokezi kwa njeo ya -hu- (wakati wa mazoea)
Njeo hii ya **hu-** husimama mwanzo wa sentensi.
Njeo ya **hu-** haitanguliwi na viambishi nafsi au viambishi vya Ngeli kama nilivyoeleza nyuma kuwa njeo ya mazoea hutanguliwa na viwakilishi nafsi au Nomino.

**Jadweli (c)**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mimi | | la | mkate |
| Wewe | | fa | |
| Yeye | Hu | Ja | maziwa |
| Sisi | | nywa | kazini |
| Nyinyi | | wa | nyumbani |
| Wao | | nya | chooni |

**Jadweli (d)**

| | | |
|---|---|---|
| Ng'ombe | | la majani |
| Watu | Hu | fanya kazi ili kuishi |
| Samaki | | ishi mjini |

Katika hali ya uyakinishi wa njeo ya **na**, **li, me, ta** zinapofuatwa na viambishi au vitenzi vifupi kama kuja, kuwa, kula, kufa, kunywa. Vitenzi hivi hubakishwa viambishi visivyo na ukomo **Ku** (Iinfinity).

Mfano
Ninakula
Nilikula
Nimekula
Nitakula

Njeo ya **hu-** itapofuatwa na vitenzi vifupi viambishi visivyoukomo **hu-** hudindishwa na kubakia mzizi wa kitenzi

Mfano
i) Ng'ombe hula majani
ii) Viumbe hunywa maji
iii) Wageni wengi huja Zanzibar

**Uyakinishi wa –Nge-**

Kulingana na Kiswahili, darasa la saba **–Nge**- ni kiungo kinachotumika kumaanisha kuwa vitendo viwili

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| A | | | -ye | Ndiye |
| WA | | | -o | Ndio |
| KI | | | - cho | Ndicho |
| VI | | | -vyo | Ndivyo |
| U | | | -yo | Ndio |
| I | | | -o | Ndio |
| U | NDI | + | -yo | Ndiyo |
| ZI | | | - zo | Ndio |
| I | | | -yo | Ndiyo |
| Z | | | - zo | Ndizo |
| LI | | | - lo | Ndilo |
| YA | | | -yo | Ndiyo |
| PA | | | -po | Ndipo |
| KU | | | -ko | Ndiko |
| MU | | | -mo | Ndimo |

vinategemeana na kuonyesha uwezekano wa vitu hivyo kutendeka.

Mfano:
– Nge
A- Nge—ingia, tunge- simama

-Ngali

Katika wakati uliopita kulingana na Wanga (2001) Ngeli ya **nge** hubadilika na kuwa Ngali au Ngeli

Mfano
i) Ningalijua, ningalikuambia
ii) Wangalipendana, wangalioana.

Kulingana na Wilson kiambishi Ngali kinatumika kuonyesha kuwa hakuna uwezekano wa kitendo kutokea kama ilivyo kwa Nge.

Mbali na kiambishi hiki cha ushuruti kiambishi kingine cha ushuruti ni **Ki**.

Kulingana na Wangat K**i** kinaonyesha matumizi ya baadae. **Ki,** hii pia inaonyesha ulazima wa kitu fulani ili kitendeke katika hali ya hii, **ki** aina hii inafuatiwa na njeo ya **'ta'**

Mfano:
i) Ukija nitaondoka
ii) Ukiimba nitacheza
iii) Wakila chakula bora watakuwa na afya

Pia kimuundo **ki,** inaweza kufuatiwa na hali ya ushauri.

Mfano:
i) Ukija ninunulie matunda
ii) Ukila uoshe mikono
iii) Ukirudi Libya nisalimie wazee wako.

**Uyakinishi wa kihusishi cha wakati –Po**

Kulingana na Kiswahili kwa darasa la saba (1989) -**Po**- ya wakati ikitumika pamoja na kitenzi huonyesha kuwa kitendo fulani kimefanyika kikionyeshwa na kitendo fulani.

Kihusishi **–po-** kikitumika pamoja na kitenzi huonyesha.

i) Kitendo fulani kilifanyika kikafuatiwa na kingine

Mifano:
i) Aliponitafuta alinipata
ii) Uliponiita niliitika
iii) Tulipofanya bidii tulifaulu

ii) Kitendo fulani kitafanyika na kitafuatwa na kingine

Mifano:
i) Nitapofaulu mtihani wa darasa la nane. Nitafurahi
ii) Ufisadi utapungua wananchi watakapokataa hongo

iii) Kitendo hufanyika na kufuatwa na kitendo au jambo jingine

Mifano:
i) Mwalimu aingiapo darasani, wanafunzi hutulia
ii) Ukimwi utajwapo, wengi hubabaika

**Uyakinishi katika hali ya ushauri**

Kulingana na Wilson hali ya ushauri huundwa kwa kudondosha kiambishi kisoukomo **ku-**.

Pia zungumza Kiswahili Hatua ya kwanza anaonyesha kuwa. Hali ya ushauri hutumika katika mazungumzo ya ana kwa ana katika hali ya Umoja na katika hali ya wingi

Mfano:

**Jadweli (d)**

| **Kitenzi** | **Hali ya Ushauri** | |
|---|---|---|
| | **Umoja** | **Wingi** |
| Kusoma | Soma | Someni |
| Kupika | Pika | Pikeni |
| Kulala | Lala | Laleni |
| Kufikiri | Fikiri | Fikirini |
| Kujibu | Jibu | Jibuni |
| Kuleta | Lete | leteni |

Kimuundo mifano hii inaonyesha vitenzi vyenye asili ya kibantu vinavyomalizikia na **'a'** katika wingi **'a'** hubakidilika na kumalizia –**eni.**

**Soma - Someni**

Vitenzi vya kigeni huongeza **'ni'**

i) Fikiri - fikirini
ii) Haribu - haribuni
iii) Kiri - kirini
iv) Samehe - sameheni

**Uyakinishi wa hali ya msisitizo Ndi-**

Kulingana na kiswahili Hatua ya Pili kiambishi **ndi-** cha msisitizo hutumika katika kusisitiza jambo au kutilia mkazo jambo fulani kiambishi hiki hubadilika umbo kulingana na kiambishi ngeli, ambacho kwa kawaida

hupachikwa mbele ya mzizi.

Mfano

**Jadweli (e)**

**KIAMBISHI MSISITIZO**

**Uyakinishi wa Ngeli.**

Majina katika lugha ya kiswahili yamegawika katika ngeli mbali mbali. Viambishi vya ngeli katika hali ya uyakinishi husimamia jina la ngeli yenyewe.

Mfano wa Ngeli zote ni kama ifuatavyo:-

A – WA
KI – VI
U – I
U – ZI
I – ZI
LI – YA
PA- KU – MU

i) A ni kiambishi awali nafsi ya kwanza uyakinishi umoja

WA ni kiambishi awali nafisi ya kwanza uyakinishi wingi

ii) KI ni kiambishi cha umoja

VI ni kiambishi cha wing kinachomuisha majina ya vitu

iii) U ni kiambishi ngel umoja

I ni kiambishi ngeli wingi

iv) U ni kiambishi ngeli umoja

ZI ni kiambishi ngeli wingi

iv) I ni kiambishi ngeli umoja

ZI ni kiambishi ngeli wingi

vi) LI ni kiambishi ngeli umoja

YA ni kiambishi ngeli wingi

Vii) PA ni kiambishi ngeli mahali, karibu

KU ni kiambishi ngeli cha mahli, mbali, kwa ujumla

MU ni kiambishi ngeli cha mahali, ndani

**UYAKINISH I WA NGELI YA KITENZI NOMINO (KU…)**

Ngeli ya Kitenzi Nomino **Ku…..**

Inajumuisha majina yote yatokanayo na Kitenzi.

Mfano, kuimba, kucheza, kusoma na kadhalika.

Mtafiti amegundua kuwa wanasarufi wameingiza ngeli hii katika orodha ya ngeli za majina kutokana na kuathirika kwake kwa baadhi ya vipashio vya sentaksia kama vitenzi, vivumishi, vimilikishi na kadhalika.

Hali hii inajidhihirisha wazi wazi katika upatanisho wa kisarufi kwa mfano:

i) **Ku**imba **ku**memtajirisha
ii) **Ku**faulu mtihani **ku**limfurahisha
iii) **Ku**subiri ni **ku**zuri

Hebu tunagalie mifano katika jadweli lifuatalo:

**Jadweli (f)**

| **VIVUMISHI** | **VIWAKILISHI** |
|---|---|
| - zuri – kuzuri | -angu kwangu |
| ku + - baya – kubaya | -ako kwako |
| -dogo – kudogo | ku + -ake kwake |
| -kubwa – kukubwa | -etu kwetu |
| | -ao kwao |

**UYAKINISHI WA NJEO YA WAKATI WA SASA (-A-)**

Kwa baadhi ya vipashio cha sentensi kulingana na Wangat (2001) anaonyesha kuwepo kwa njeo ya (-A-) wakati wa sasa unaofanya kazi kama na, kulingana na maelezo yake mara nyingi hutumika katika mazungumzo zaidi.

Kimuundo ngeli hii hujitokeza kama ifuatavyo:-

Ni + a - nasoma
U + a - wasoma
a + a - asoma
m + a - mwasoma
wa + a - wasoma
U – 1 (M – MI)
u + a - waanguka
i + a - yaanguka
KI – VI
ki + a - chaanguka
vi + a - vyaanguka
U – ZI
u + a - waanguka
zi + a - zaanguka
I + a - yaanguka
zi + a - zaanguka
li + a - laanguka
ya + a - yaanguka
pa + a - panukia vizuri
ku + a - kwanukia vizuri
m + a - mwanukia vizuri
KU
Ku + a kusoma kwaendelea

**UYAKINISHI WA KITENZI KUWA NA**

Mgulu (1999) Anaonyesha kitenzi hili katika kazi yake ya "mtaala wa Isimu" amelezea kuwa kitenzi hiki ni muhimu sana katika mazungumzo ya lugha ya Kiswahili na kitenzi hiki kinachojitokeza katika maumbo tofauti kulingana na wakati, kwa mfano wakati wa sasa.

**(g) Jadweli**

| | |
|---|---|
| Ni + na | Nina |
| U + na | Una |
| A + na | Ana |
| Tu + na | Tuna |
| M + na | Mna |
| Wa + na | Wana |

Katika jadweli hili kiambishi cha umiliki -**na** kinatanguliwa na kiambishi nafsi cha ngeli ya

A – WA
KI Kina
VI Vina
U Una
I Ina
U Una
ZI Zina
I NA Ina
ZI Zina

| | |
|---|---|
| LI | Lina |
| YA | Yana |
| PA | Pana |
| KU | Kuna |
| MU | Muna |

**UKANUSHI KATIKA SARUFI YA KISWAHLI**

Sura hii inakusudia kuzungumzia ukanushi unavyojitokeza katika lugha ya Kiswahili. Mtafiti amechunguza kazi anuwai za wataalamu zilizozungumzia ukanushi wa lugha ya Kiswahili.

**UKANUSHI WA VIAMBISH NAFSI**

Zungumza Kiswahili hatua ya kwanza amevitaja viambishi vya ukanushi kulingana na nafsi kama inavyojionyesha katika Jadweli.

| VIAMBISHI YAKINISHI | VIAMBISHI KANUSHI |
|---|---|
| Ni | Si |
| U | Hu |
| A | Ha |
| TU | Hatu |
| M | Ham |
| WA | Hawa |

Kulingana na Jadweli hii viambishi vya ukanushi ni **Si** na **Ha.**

**UKANUSHI WA VITENZI SHIRIKISHI**

Kulingana na Mohammed ukanushi wa vitenzi shirikishi ni **Si**

| **YAKINISHI** | **Kanushi** |
|---|---|
| NDI - | Si- |
| -LI- | Si- |
| -KO | **Si-** na **Ha** kulingana na nafsi |
| -PO | Si- |
| -MO | Si- |
| - NA | 'Ha" katika mazingira ya pana kuna mna |
| -YU | Si- |
| -U | Si- |

Kwa ujumla viambishi vya ukanushi kulingana na Jadweli hilo ni **Si** na **Ha.**

**UKANUSHI WA KITENZI –KUWA-**

Ukanushi wa kitenzi -**kuwa-** katika wakati wa sasa. Katika wakati wa sasa kitenzi **kuwa-** hubadilika na kuwa **Si**

Mfano

i) Mimi si mwalimu
ii) Yeye si Mlibya
iii) Wewe si Mohammed

**UKANUSHI WA KITENZI –KUWA - KWA WAKATI ULIOPITA, UJAO NA ENDELEVU**

Katika nyakati hizi kitenzi **-kuwa-** huchukuliwa kiambishi awali **–ha-**

**Jadweli (h)**

Angalia Jadweli lifuatalo:

| YAKINISHI | UKANUSHI |
|---|---|
| Likuwa | Hakuwa |
| Takuwa | Hatakuwa |
| Mekuwa | Hajawa |

Ukiangalia jadweli hili inadhihirisha wazi kuwa **'Ha'** ni kiambishi cha ukanushi

Kimuundo ukanushi katika wakati uliopita kiambishi cha Ukanushi hufuatatwa na kitenzi **kuwa.** Aidha katka wakati ujao kiambishi **'ha'** hufuatwa na Njeo ya **'ta'** pamoja na kitenzi **kuwa** na kufanya **Ha**takuwa. Katika wakati endelevu '**me'** ya uyakinishi hubadilika na kuwa –**ja-.**

Mfano, -**me**kuwa – **ha**jawa

**UKANUSHI WA NJEO YA MAZOEA HU-**

Kama nilivyoonesha katika uyakinishi njeo hii imeelezwa na wataalamu wengi, kuwa ni muhimu katika lugha ya Kiswahili. Kulingana na Wilson ukanushi wa –**Hu-** hautafautiani na ukanushi wa njeo ya wakati wa sasa.

**Jadweli (i)**

Angalia jadweli lifuatalo

Mfano

| NAFSI | YAKINISHI | KANUSHI |
|---|---|---|
| Mimi | hula matunda | Mimi sili matunda |
| Wewe | hula matunda | Wewe huli matunda |
| Yeye | hula matunda | Yeye hali matunda |
| Sisi | hula matunda | Sisi hatuli matunda |
| Nyinyi | hula matunda | Nyinyi hamli matunda |
| Wao | Hula matunda | Wao hawali matunda |

Kutokana na jadweli hili mtafiti amegundua kuwa hakuna tafauti ya kimatumizi kati ya njeo ya **'na'** wakati wa sasa na **hu-** ya mazoea.

Angalia jadweli **(j)** hapo juu.

**UKANUSHI WA USHURUTI –NGE-**

Kulingana na Wangat ukanushii wa viambishi vya ushuruti –**nge-** katika wakati wa sasa na wakati uliopita ni **si.**

Mfano:

| **UYAKINISHI** | **UKANUSHI** |
|---|---|
| Ningekuja | Ni**si**ngekuja |
| Ningalikuja | Ni**si**ngalikuja |

Kimbishi ch ukanushi kinajitokeza baada ya kiambishi nafsi cha mtenda

**Ukanushi wa kiambishi –Ki- cha Ushuruti**

Wangat anaelezea kuwa kiambishi –**ki-** cha ushuruti hubadilika na kuwa –**sipo-**

Wangat anaendelea kusema kuwa katika hali ya ukanushi kiambishi hakitanguliwi na kiambishi kanushi cha mtenda, lakini kionyeshi cha ukanushi –**sipo-** hupachikwa baina ya kiambishi cha mtenda na mzizi wa kitendo katika kuthibitisha hilo Wangat anaonyesha mifano ifuatayo:

i) Usiposoma kitabu hiki vizuri hutajua Kiswahili
ii) Usipofika mjini usinipigie simu
iii) Usipokula mkate usilale

**UKANUSHI WA KIHUSISHI CHA WAKATI –PO-**

Kulingana na Wilson kihusishi cha wakati **–po-** katika hali ya ukanushi hubadilika na kuwa –**sipo-** kiambishi hiki hutanguliwa na viambishi ngeli

Mfano:

| | | |
|---|---|---|
| Nilipofika | - | Nisipofika |
| Ulipofika | - | Usipofika |
| Alipofika | - | Asipofika |
| Tulipofika | - | Tuisipofika |
| Mlipofika | - | Msipofika |
| Walipofika | - | Wasipofika |

**UKANUSHI WA HALI YA USHAURI**

Kulingana na Wilson hali ya ushauri, Kiambishi kanushi cha hali ya Ushauri ni **Si** kiambishi hiki hupachikwa

baina ya kiambishi nafsi na mzizi.
Mifano:

Nisome - Nisisome!
Ninywe - Nisinywe!
Nije - Nisije!

**UKANUSHI WA VIAMBISHI VYA MSISITIZO**

Kulingana na Mohammed viambishi vya msisitizo vyote katika hali ya ukanushi hubadilika na kuwa –**Si-**

**Ndi -Si**

Mfano

| **Ngeli za majina** | **Yakinishi** | **Kanushi** |
|---|---|---|
| A | Ndiye | Siye |
| WA | Ndio | Sio |
| KI | Ndicho | Sicho |
| VI | Ndivyo | Sivyo |
| U | Ndio | Sio |
| I | Ndiyo | Siyo |
| ZI | Ndizo | Sizo |
| I | Ndiyo | Siyo |
| ZI | Ndizo | Sizo |
| LI | Ndilo | Silo |
| YA | Ndiyo | Siyo |
| PA | Ndipo | Sipo |
| KU | Ndiko | Siko |
| MU | Ndimo | Simo |

**UKANUSHI WA KITENZI KUWA KWA WAKATI WA SASA, UJAO, ULIOPO NA WAKATI ENDELEVU**

Katika wakati wa sasa viambishi vya ukanushi ni **S**i na **Ha**

Ni - Si
U - Hu
A _ Ha
TU - Hau
M - Ham
WA - Hawa

**Wakati uliopita**
Nilikuwa na – sikuwa na
**Wakati ujao**
Nitakuwa na – sitakuwa na
**Wakati endelevu**
Nimekuwa na – sijawa na

Mtafiti amegundua kuwa kimuundo kitenzi **kuwa** na hubeba kiambishi **Si** na **Ha** katika ukanushi.

**UKANUSHI WA NGELI YA KITENZI NOMINO (KU….)**

Kulingana na Wilson, ukanushi wa Ngeli ya Kitenzi Nomino (KU….) hutokea kwa kuingizwa kiambishi **–to-** baina ya **ku** na mzizi wa kitenzi. Angalia jadweli (k)

**Jadweli (k)**
**Mfano**

| **YAKINISHI** | **KANUSHI** |
|---|---|
| Kuimba | Kutoimba |
| Kufikiri | Kutofikiri |
| Kula | Kutokula |

Katika ukanusi ngeli hii haichukui viambishi vya ukanushi kama ilivyo katika ngeli nyengine pia kwa vitenzi vifupi, ngeli hii haidondoshi kiambishi kisicho ukomo (Ku…)
Mfano:
Kula - kuto**ku**la
Kufa - kuto**ku**fa

**HITIMISHO**

Utafiti huu ulidhamiriwa kuonyesha uyakinishi na ukanushi katika lugha ya Kiswahili. Imebainisha kuwa uyakinishi katika lugha ya Kiswahili hudhihirika katika Ngeli za majina, viambishi na Njeo za wakati.

Wakati katika ukanushi hubadilika na kubeba viambishi vya ukanushi kulingana na
Ngeli.
Viambishi muhimu katika ukanushi ni:-
**'Si**' ambapo husismamia nafsi kwanza umoja
**'Hu'** - husimamia nafsi ya pili umoja
**'Ha'** - husimamia nafsi ya tatu umoja
**'Hatu'** - husimamia nafsi ya kwanza wingi.
**'Ham'** - husimamia nafsi ya pili wingi
**'Hawa'** - husimamia nafsi ya tatu wingi.

Hata hivyo utafiti umebainisha kuwa kuna hali katika sarufi ya kiswahili ambazo hazibebi viambishi awali vya ukanushi. Pia sentensi za ushuruti nazo hazibebi viambishi awali vya ukanushi. Hata hivyo kiambishi kinachobainisha ukanushi katika hali na sentensi za ushuruti ni '**Si'** wa uwepo wa kiambishi hiki katika tungo za aina hii unadhihirisha wazi kuwa kiambishi –'**Si'**- ni muhimu sana katika ukanushi pamoja na mofimu '**Ha'**. Ukanushi wowote wa Kiswahili kwa njia moja au nyengine ni lazima ubebe '**Si'** au mofimu **'Ha'** katika uhanushi.

**HITIMISHO**

Utafiti huu ulidhamiriwa kuonyesha uyakinishi na ukanushi katika lugha ya Kiswahili. Imebainisha kuwa uyakinishi katika lugha ya Kiswahili hudhihirika katika Ngeli za majina, viambishi na Njeo za wakati.

Wakati katika ukanushi hubadilika na kubeba viambishi vya ukanushi kulingana na
Ngeli.
Viambishi muhimu katika ukanushi ni:-
**'Si**' ambapo husismamia nafsi kwanza umoja
**'Hu'** - husimamia nafsi ya pili umoja
**'Ha'** - husimamia nafsi ya tatu umoja
**'Hatu'** - husimamia nafsi ya kwanza wingi.
**'Ham'** - husimamia nafsi ya pili wingi
**'Hawa'** - husimamia nafsi ya tatu wingi.

Hata hivyo utafiti umebainisha kuwa kuna hali katika sarufi ya kiswahili ambazo hazibebi viambishi awali vya ukanushi. Pia sentensi za ushuruti nazo hazibebi viambishi awali vya ukanushi. Hata hivyo kiambishi kinachobainisha ukanushi katika hali na sentensi za ushuruti ni '**Si'** wa uwepo wa kiambishi hiki katika tungo za aina hii unadhihirisha wazi kuwa kiambishi –'**Si'**- ni muhimu sana katika ukanushi pamoja na mofimu '**Ha'**. Ukanushi wowote wa Kiswahili kwa njia moja au nyengine ni lazima ubebe '**Si'** au mofimu **'Ha'** katika uhanushi.

**MAREJEO**

*Habwe, J, & Karanja, P (2004) Misingi ya Sarufi ya Kiswahili, Nairobi:*
*Phonix Publichers Ltd.*

*Massebo, J, & Nyangwina, N (2002) ; Kiswahili kidato cha 3 na 4 Dar es Salaam*
*Afro Plus Industries Ltd.*

*Mgullu, R, S (1955): Mtaala wa Isimu, Fonetiki, Fonolohi na Mofolojia ya Kiswahili :*
*Longhorm Publishers*

*Mohammed, M. (2001) Modern Swahili Gra Education Publishers mmer, Dar es Salaam East African Educaton Publishers*

*Mohammed, A.M.A.T (2013) Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania*
*Tofauti Ya Viambishi Kanusha Kati Ya Kiwahili Na Kiairabu.*

*Kiswahili Darasa la Saba (1998) Kenya Literature Bureau. Nairobi.*

*Wilson, P, M (1991) Simplified Swahili, Longman Group Uk Limited, Longman House, Burnt mill, Harlow, England.*

*Zungumza Kiswahili – Hatua yaKwanza (2003) –SUZA Educational Book Publishers Ltd Tanzania.*
*Zungumza Kiswahili – Hatua ya Pili (2003) – SUZA Educational Book Publishers Ltd Tanzania.*